

**Naswaha Ya Shaykh Abdul-Muhsin al- Abbâd kwa  
Shaykh Rabi bin Hadi al-Madkhlali (حفظهما الله)**

---

رَفَقًا أَهْلَ السُّنَّةِ بِأَهْلِ السُّنَّةِ

**KUWENI NA UPOLE, ENYI WATU  
WA SUNNAH,**

**NA WENZENU KATIKA SUNNAH.**

Mwanzoni mwa mwezi wa Ramadhân ya mwaka wa 1423H, miezi sita kabla ya kuchapishwa *Rifqan Ahl as-Sunnah bi Ahl as-Sunnah*, nilituma barua ya naswaha kwa mmojawapo wa watu waliowaathiri vijana wa Watu Wa Sunnah.<sup>1</sup> Akanijibu kwa unyenyekevu katika barua kwa kumuomba Allâh amnufaishe kwa naswaha kama hiyo na akasema yakwamba amemnaswihi mwenzake niliyemkusudia katika barua hiyo.<sup>2</sup> Namuomba Allâh atuafikiye mimi na yeye, na vilevile ndugu zetu wote miongoni mwa Watu Wa Sunnah, kufuzu ni kwa kila chenye kurudi kwenye kheri na mwisho mwema, na Atuepushe sote na kila lijalo na shari na mwisho mbaya duniani na akhera, kwa hakika Yeye ni mwenye kusikiya na mwenye kujibu. Na yafuatayo ni yaliyokuwemo katika barua [yangu] niliyomtumia.

Kwa hivyo, hakika nayaandika maneno haya kwa heshima zenu, maneno haya nikitumai yakwamba mutayakubali maneno haya kwa macho ya mazingatio, kwani «dini ni kunasihiana» na «mu'min kwa mu'min mwenzake ni kama mfano wa jengo; latiliana nguvu lenyewe kwa lenyewe». Na miongoni mwa haki ya Muislamu kwa Muislamu mwenzake ni kumnaswihi na kusaidiana nae kwa wema.

1. Pindi tulipokutana na wewe katika mkutano ulomalizika hivi karibuni, ulinitajia yakwamba wewe ni mkubwa wangu kwa umri; na mimi katika masiku kama

---

<sup>1</sup> [Mf]: yaani; Shaikh Rabî' bin Hâdî al-Madkhalî.

<sup>2</sup> [Mf]: yaani Shaikh Fâlih bin Nâfi' al-Harbî.

haya nimeshaingia katika miongo ya thamanini<sup>3</sup> na kulingana na haya, wewe umenitangulia mimi katika muongo huu. Kwahiyo kama ilivyo, kwa hakika kutokana na ualimu wangu kwako wewe katika mwaka wa 1381H na yalofuata baada ya hapo, inakuwa ni kutoka kwa walio wakubwa kupokea kutoka kwa walio wadogo.<sup>4</sup> Na mfano wangu mimi na wewe kuna haja ya kushughulishwa na kila lenye kuleta uharibifu baina ya Watu Wa Sunnah kwa Ilmu yenye manufaa.

2. Kitambo kidogo, niliwahi kusikia neno fulani kutoka kwako: yakwamba umepata usumbufu uliokutoa katika njia ya kujishughulisha na Qur'án na kuizingatia juu ya ufahamu wake kwa kujishughulisha na Hadeeth na watu wake<sup>5</sup>. Sasa mimi nasema yakwamba umeshughulishwa mbali na Qur'án na Hadith kwa kuanza kuwazungumza baadhi ya Watu Wa Sunnah, na wengineo. Katika yaliyokushughulisha wewe badala ya kushughulika na 'Ílmu ya Kitâbu na Sunnah natija yako ya ki-ilimu ikawa ni chache katika siku hizi za mwisho. Na hapana shaka kule kupambana kwako na wasiokuwa katika Watu Wa Sunnah na [pamoja na] wale wenye alama za fitna, ni kuwatweza wanavyuoni kwa madai ya ukosefu wa kuyafahamu [matukio] ya kilimwengu "*fiqh ul-Wâqi'*", yametokea kutoka kwao - [mambo ambayo] ndipo mahali pake hapa. Lakini jambo ambalo hapa si mahala pake na si sawa ni kule kuelekeza nyuso zenu na wakati wenu katika kufuatilizia baadhi ya makosa ya watu ambao ni katika Watu Wa Sunnah na kuwakejeli kwa sababu ya kutoafikiana na nyinyi kutokamana na baadhi ya rai ambazo mulizoshikamana nazo. Mfano wa watu kama hawa haifai kujishughulisha sana na wao. Na itakapotokea kutaja baadhi ya makosa yao, basi haifai kujishughulisha na makosa yao na kuyakariri mpaka mukayafanya ni hadithi au mazungumzo ya mikao. Kisha wakati wa mijadala, ikapatikana miongoni mwenu hasira na kupaaza sauti zenu - Hakika hilo, na kuongezea katika yale yapatikanayo mambo ya hatari kuna kuathirika kwa swiha ya mtu.

3. Imekuwa ni mashuhuri katika masiku kama haya kutaja mas'ala ya *Jarh* na *Ta'deel* na kuwazungumza baadhi ya Watu Wa Sunnah na wengineo. Kusambaa kwa mas'ala hayo katika *Internet* ni katika yaliyo sababisha kuja [kwa mfululizo] maswali kutoka Uropa, Amerika, Afrika Ya Kaskazini na [miji] mengineyo, kuhusu baadhi ya wale ambao kujeruhiwa kwao kulitokamana na wewe na Sheikh ...<sup>6</sup> pamoja na kuyapanua maneno ya Sheikh ...<sup>7</sup> katika kuvunja heshima ya baadhi ya mashekhe na baadhi ya wanafunzi wa ilimu, ndani ya miji na ugenini - ambao Allâh amewanufaisha

---

<sup>3</sup> [Mf]: yaani katika miaka ya 70. Alipokuwa ni miongoni mwa wanafunzi wa Shaikh 'Abdul-Muhsin alipokuwa ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu Cha Madīnah, Shaikh Rabī' bin Hādī ni mkubwa wa umri kwa takriban mwaka au Zaidi kuliko Shaikh 'Abdul-Muhsin. Shaikh Rabī' aliutaja uhakika huu hadharani wakati wa kilele cha ghasia zilizozuka ambazo zilizotajwa hapo juu, na habari hizo zinaweza kupatikana kwenye baadhi ya majukwaa ya internet.

<sup>4</sup> [Mf]: Yaani; (Kwa lugha ya kiarabu): *Riwâyah al-Akâbir án al-Asâghir* - Maana yake; Riwaya za walio wakubwa kutoka kwa walio wadogo. [a] Kama ilivyo [ilivyotajwa] katika *Nuzhah an-Nadhr Sharh Nukhbah al-Fikr* - Cha al-Hafidh ibn Hajar, "Wakubwa wanapokea kutoka kwa wadogo ni upokeaji wa mwenye kupokea kutoka kwa walio chini yake kwa umri (kuonana yaani; kuonana na mashekhe), au kwa daraja.

<sup>5</sup> [Mf]: Yaani; Wapokezi wake.

<sup>6</sup> [Mf]: Tizama maandishi ya chini No.1 nukta hizo (...) zilitumiwa na Sheikh 'Abdul-Muhsin kwenye mahali mwa kutajwa jina la Sheikh muhusika.

<sup>7</sup> ibid

watu kutokamana na mihadhara yao na vitabu vyao, kwa kuwatahadharisha watu dhidi yao; na yenye kuja juu ya hayo yanayosababisha kujitenga nao na kuteta, na Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema:

« بشروا، ولا تتفروا، ويسروا ولا تعسروا »

“Wapeni watu bishara njema wala musiwakimbize, wafanyieni watu usahali wala musiwafanyie uzito.”<sup>8</sup>

Na mwenye kukosea miongoni mwa Watu Wa Sunnah, siku zote hufanya bidii katika kushajiisha juu ya kheri, pamoja na kutanabahishwa juu ya kosa lake, iwapo kosa lake liko wazi, lakini watu hawajitengi nae wala hawampigi vita na wala watu hawatahadharishwi kutokamana na kufaidika kutoka kwake.

Ingawaje mimi naamini yakwamba hukubaliani nae kuhusiana na baadhi ya maneno yake kuwahuu watu fulani, kwa sababu ya ushirikiano ulioko baina yako na Sheikh ...<sup>9</sup> na mnasaba wa ukosoaji kwako wewe na yeye, mambo yasiyotoka kwako huwenda yakadhaniwa yakwamba ni yako. Kutokamana na hayo, matarajio yangu kwako wewe, ni kwamba usijishughulisha nafsi yako na kuwakosoa miongoni mwa Watu Wa Sunnah, na kuwa msimamo wako kumuhusu yeye una mipaka yake kiasi cha kwamba wanafunzi wa ilimu na wengineo, walio mijini na ugenini, wawe wamesalimika na kujishughulisha na “yasemekana” na “amesema” na uulizaji wa maswali baada ya hayo: “Wasemaje kuhusu ukosoaji wa fulani na fulani”, au “fulani na fulani kwa fulani na fulani”, au “fulani na fulani” (hata kama hakuna mafungamano yoyote baina yako na mtu huyu)? Wewe ni mtu maarufu kwa juhudi katika masomo na kufundisha, na una vitabu vyenye manufaa. Wewe umewashinda wenzako katika siku za masomo na umeandika vitabu vizuri kuhusiana na ilimu. Amma yeye ...<sup>10</sup>, alikuwa ni miongoni mwa wanafunzi wa mwisho katika darasa na daraja yake ilikuwa katika kupita [mtihani] ni ‘nzuri’<sup>11</sup>. Yeye hakuwa na Cheo katika ilimu, hana vitabu alivyoandika, na shehena la bidhaa zake limejaa matusi na kuwavunjia watu heshima zao. Katika siku ya Hudaibiyyah, una mfano mwema wa kuiga kutoka kwa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم); mpaka baadae wale waliojuta kwa yaliyotokamana na wao, wakasema baadhi yao, “Enyi watu, zituhumuni rai zenu katika dini!”

Namuomba Allâh (عزَّ وجلَّ) atuafikie sote katika yenye kumridhisha Yeye, atuonyeshe haki kuwa ni haki na atuafikie kuifuata, na atuonyeshe bâtil kuwa ni bâtil na atuafikie kuiepuka, hakika Yeye ni Mwenye kusikiya na Mwenye kujibu.

<sup>8</sup> Muslim, Abu Dâwud, Ahmad na wengineo

<sup>9</sup> ibid

<sup>10</sup> [Mf]: Tizama maandishi ya chini No.1

<sup>11</sup> [Mf]: Kwa kiarabu: Jayyid - nzuri (kama ilivyo kwenye usahihishaji wa mitihani, hiyo si kama mtu kufuzu kwa alama bora ya ‘Mumtâz’)

Kila Sifa njema zimthubutukie Allâh, Bwana wa viumbe vyote; na swala na salamu na baraka za Allâh zimfikie mja wake na Mtume wake, Mtume wetu Muhammad ( صلى الله عليه وسلم ) na jamaa zake na Maswahaba wake.

[Mf]: Mfasiri  
Imefasiriwa na Muhammad Awadh Salim Basawad